

Je, ninapaswa kupimwa lini? Kukaribiana

MANUKUU

[Muziki wa Kusisimua]

[Masimulizi]

Je, unapaswa kupimwa COVID-19 lini?

Ulienda nyumbani kwa rafiki siku ya Ijumaa usiku kushiriki chakula cha jioni na michezo. Ulikaa karibu na rafiki ambaye ana COVID-19 lakini bado hajajua. Uligundua Jumapili alasiri kuwa rafiki yako ameambukizwa COVID-19.

Unapaswa kupimwa siku tano kamili baada ya kukaribiana na mtu ambaye ana COVID-19. Katika tukio hili, ulikaribiana na mgonjwa siku ya Ijumaa, kwa hivyo unapaswa kupimwa Alhamisi.

Ukikaribiana na mtu aliyeambukizwa COVID-19, tembelea ukurasa wa tovuti wa MDH kuhusu Kukaribiana au Kuhatarishwa na COVID-19 upate maelezo kuhusu urefu wa muda unaopaswa kuva barakoa ukiwa karibu na wengine, na mengineyo.:

<https://www.health.state.mn.us/diseases/coronavirus/close.html>.

Ukianza kuhisi mgonjwa, pimwa haraka iwezekanavyo.

Ili upate maelezo zaidi kuhusu nyakati nyingine unazopaswa kupimwa, na mahali pa kupimiwa, tembelea ukurasa wa tovuti ya MDH ya Kupimwa COVID-19:

<https://www.health.state.mn.us/diseases/coronavirus/testsites/index.html>.

[Muziki wa kusisimua]

Minnesota Department of Health
Communications Office
PO Box 64975
St. Paul, MN 55164-0975
651-201-4989
health.communications@state.mn.us
www.health.state.mn.us

12/9/2022 (Swahili)

Ili upate maelezo haya katika muundo tofauti, piga simu: 651-201-4989